

MAR - KIM UNIPLAST

W LID

Japan kufundisha madaktari wa mifupa

Elizabeth Edward, Mwananchi
eedward@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Changamoto ya uhaba wa madaktari bingwa wa mifupa na mishipa ya fahamu hueda ikawa historia baada ya serikali ya Japan kukubali ombi la kutoa mafunzo ya kuwatengeneza wataalam hao.

Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Umyy Mwalimu amesema kwa sasa kuna changamoto ya upungufu wa madaktari hao ambao kwa Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (Moi) wapo madaktari saba wa mishipa wakati wanaohitajika ni 13.

Japan itaisaidia Tanzania katika kujenga uwezo wa matibabu ya kibingwa ya mifupa na mishipa ya fahamu.

Upande wa madaktari wa dawa za usingizi, Umyy alisema wapo watano wakati mahitaji kwa Moi peke yake ni 15.

Kutokana na hali hiyo, Umyy amemuomba rais wa taasisi ya Japan inayoshughulikia masuala ya uchumi na maendeleo katika bara la Afrika (Afreco), Tetsuro Yani kuisaidia Tanzania kupata wataalamu wa kutosha.

Alisema wataalamu wakiwepo wa kutosha itasaidia Tanzania kuzidi kuboresha huduma za afya



"Tunachohitaji ni kuboresha matibabu ya mifupa na mishipa ya fahamu."

Umyy Mwalimu

zinazotolewa ili ziwe za uhakika zaidi.

"Tunajua wenzetu Japan wako mbele kwenye upande wa teknolojia ndiyo maana tunaomba watusaidie kwa kuwafundisha madaktari wetu wakabobee katika matibabu hayo ya kibingwa.

"Tunachohitaji ni kuboresha matibabu ya kibingwa kwenye mifupa na mishipa ya fahamu na hilo litafanikiwa tukiwashirikisha wenzetu ambao wako mbele kwenye teknolojia," alisema Umyy.

Waziri huyo pia aliomba kushirikiana na Japan katika ujenzi wa vyumba vya upasuaji akieleza kuwa kwa Moi viko tisa wakati

mahitaji ni vyumba 13.

Ombi lingine lililotolewa na Umyy ni kuwezesha kuanzisha kituo cha utengamao kwa ajili ya kuwarudisha kwenye hali ya kawaida watu waliotibiwa baada ya kupata ajali.

Kwa upande wake, Yani alisema Serikali ya Japan iko tayari kuisaidia Tanzania katika eneo hilo ili kuunga mkono jitihada zinazoendelea kufanywa na serikali katika kuboresha huduma za afya.

Sanjari na Moi, alisema Japan itashirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kujenga kituo cha matibabu pamoja na kuanzi-

OMBI

Waomba uamuzi kujitoea korti ya Afrika uangaliwe

Elias Msuya, Mwananchi
emsuya@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Taasisi mbili-tandao wa Watetezi za Haki binadamu (THRDC) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) zimeomba Serikali ifikirie upya uamuzi wake wa kujitoea katika azimio linaloruhusu wananchi pamoja na asasi za kiraia kupeleka malalamiko moja kwa moja mbele ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu.

Katika barua iliyosainiwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi Novemba 21, Serikali imeweka kusudio la kujiondoa kwenye kifungo cha 34(6) cha itifaki ya mahakama hiyo kinachoruhusu watu binafsi na asasi za kiraia kupeleka mashitaka, ikisema azimio hilo limekuwa likitumika kinyume na mipaka iliyowekwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa alisema Serikali imechukua uamuzi huo bila kushirikisha wadau na bila kuweka bayana mipaka inayovukwa.

"Kujitoea bila kushirikisha wadau wa azimio kumezua sintofahamu ukizingatia pia kuwa Serikali haikuweka bayana ni mipaka ipi ilijitokea na ni kwa namna gani imekuwa ikikiukwa," alisema Olengurumwa.

"Haijulikani ni kwa namna gani Serikali iliwahusisha wadau katika meza ya majadiliano ili kurekebisha kasoro ambazo zimekuwa zikisababisha ukiukwaji wa mipaka iliyowekwa na Serikali wakati inatia saini mkataba ulioanzisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu."

Aliomba Serikali kufikiria upya uamuzi huo wa kujitoea na ikiwezekana ibadilishe kwani inaleta taswira mbaya na inawanyima wananchi na asasi fursa ya kuifikia mahakama hiyo.



NUKUU

"Kama Serikali haitasikiliza wito wetu, tutatafakari uwezekano wa kuishitaki kwenye Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu."

Onesmo Olengurumwa

"Tunaiomba Serikali itekeleze uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu kwa nia njema ili iendelee kuhifadhi taswira ya nchi mwenyeji wa mahakama hiyo. Tunaomba ieleze umma wa Watanzania mipaka iliyowekwa wakati wa kuruhusu azimio lake na kwa namna gani mipaka hiyo imekiukwa," alisema.

Pia, ameziomba asasi za kiraia pamoja na wananchi kuendelea kuitumia Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na watu pamoja na mahakama ya Afrika Mashariki kwa kupeleka malalamiko yao

pale haki zao zinapovunjwa.

"Pia watumie kipindi hiki cha mwaka mmoja ambao Tanzania imetoa notisi kudai haki zao katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu," alisema.

Hata hivyo, alisema endapo Serikali haitasikiliza wito huo, watatafakari uwezekano wa kuishitaki Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu.

"Ikishindikana hiyo tutakwenda kwenye kamisheni kule Banjul (Gambia), kwa sababu Tume ya Haki za Binadamu ya Afrika ndiyo mama wa hii mahakama," alisema Olengurumwa.

Alisema mahakama hiyo iliundwa baada ya kuonekana tume ya haki za binadamu ya Afrika haikuwa na nafasi ya kusikiliza kesi.

Mbali na THRDC, mkurugenzi wa LHRC, Anna Henga alisema kusudio la Serikali kujitoea katika mahakama hiyo litasababisha gharama kubwa kwa wananchi kwenda kupeleka kesi zao kwenye Tume ya Haki za Binadamu ya Afrika nchini Gambia.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga. Picha na Ericky Boniphace

Dawa za ARV zampunguzia adhabu ya kifungo

Twalad Salum, Mwananchi
tsalum@mwananchi.co.tz

Misungwi. Ahmad Nonga (35), ambaye ni mkazi wa kijiji cha Misungwi mkoani Mwanza, amehukumiwa na mahakama ya wilaya kifungo cha miezi 18 jela badala ya miaka saba baada ya kuomba kupunguziwa adhabu alipoonyesha kadi ya matibabu na vidonge vya kufubaza Virusi vya Ukimwi (ARV).

Adhabu hiyo ilitolewa juzi baada ya mahakama kumkuta na hatia ya kosa la kuvunja na kuiba.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Esther Malick baada ya kumkuta na hatia ya kosa la kuvunja na kuiba.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Malick alisema kutokana na mshtakiwa kuonyesha vidonge hivyo mahakama imepunguzia adhabu ya kifungo alichostahili kufungwa.

Mapema Nonga aliiomba mahakama hiyo kumpunguzia adhabu kutokana na kuwa mgonjwa anayeishi kwa matumaini huku akitoa kadi na vidonge vya ARV pia kuongeza alikuwa anategemea na watoto na mama yake mzazi.

Mahakama baada ya kusikiliza kilio chake ilimhukumu kwenda jela miezi 18 badala ya miaka saba kulingana na adhabu ya kosa la kuvunja na kuiba.

Awali, mwendesha mashitaka mkaguzi msaidizi wa polisi, Juma Kiparo akisoma hati ya mashitaka alidai mshtakiwa alivunja duka na kuiba bidhaa zenye thamani ya Sh1.5 milioni, mali ya Winnefrida Daud, Agosti mwaka huu katika kijiji cha Mbela.



UCHAGUZI CHADEMA

Sumaye aacha fumbo

Ibrahim Yamola, Mwananchi
iyamola@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Dakika 30 zilimtosha Frederick Sumaye kuzungumzia safari yake ya kisiasa akiwa Chadema na uamuzi wa kung'oka, lakini ameacha fumbo nyuma yake.

Wakati ofisi yake ilipotuma mwaliko kwa maandishi wa habari juzi kuhusu mkutano wake wa leo, ubashiri ulikuwa mmoja tu; waziri huyo mkuu wa zamani anarejea CCM kama makada wengine waliokihama chama hicho tawala mwaka 2015, likiongozwa na mtendaji mwingine mkuu wa Serikali wa zamani, Edward Lowassa.

Lakini wakati anamaliza mkutano wake, hakuna aliyejua Sumaye anaelekea wapi baada ya kusema ataendelea kubakia kwenye siasa na yuko tayari kushirikiana na chama chochote.

Mazingira ya mkutano wake na maandishi wa habari, mtindo wa kujipa mmuda kabla ya kutangaza chama anachoenda kama alivyofanya mwaka 2015 na ulinzi wa askari wenye sare na mambo mengine, yanaweza kuwa yameacha fumbo zaidi kuhusu mustakabali wa waziri mkuu huyo wa zamani aliyeng'ara katika kampeni za mwaka 2015.

Na mwaliko wake kwa maandishi ulitumia barua iliyokuwa na nembo ya Adamu na Hawa ya Serikali, lakini akatumia nafasi hiyo kuomba radhi kwa kasoro hiyo iliyoibua ubashiri kuwa angetangaza kurejea chama tawala.

Sumaye alitumia mkutano wa jana kuelekeza shutuma kwa mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, akisema baada ya kutafakari kwa kina na kuona walioshiriki kumuangusha ni wajumbe wa Kamati Kuu, "nimelazimika kwa kulazimishwa kujiondoa Chadema kutokea leo hii na sijiungi na chama chochote cha siasa".

"Niko huru kutumika na chama chochote ikiwa ni pamoja na Chadema kwa kutoa ushauri nakadhalika," alisema Sumaye akisisitiza msimamo wake wakati akijiunga upinzani mwaka 2015 kuwa ataendelea kuimarisha upinzani.

"Najua katika kujikosha yatakuwepo maneno kama kupewa fedha na CCM au ACT-Wazalendo na kadhalika. Kama nilipokuja Chadema mlinipa fedha, basi na sasa nitakuwa nimepewa sijui na nani."

Sumaye alisema wapo watakaoumizwa na uamuzi wake, lakini akasema umechangiwa na viongozi wa Kanda ya Pwani akitumia maneno ya Biblia, "rushwa huwapofua macho hao wana-

ona na kuyapotoa maneno ya wenye haki".

Mbowe hakutaka kujibu tuhuma dhidi yake alipohojiwa na Mwananchi jana zaidi ya kusema wakati ukifika atafanya hivyo.

"Mimi ni mwanasiasa sitaacha siasa," alisema Sumaye ambaye alikuwa mmoja wa wanachama wa Chadema aliyejitosa kuwania uenyekiti wa chama hicho katika uchaguzi utakaofanyika baadaye mwezi huu.

Ujumbe kwa Mbowe

Lakini Sumaye alisema waliomtendea mabaya katika uchaguzi wa kanda walidhani wanamkomoa, "lakini wamekijengea chama mazingira ya ovyo na ya aibu".

"Mbowe najua utakuwa mwenyekiti wetu wa chama, hilo kundi lako linalojidai ndiyo 'cabinet' (baraza) yako ya ndani usipoliangalia litakuvunjia chama," alisema.

Akisoma taarifa yake kwa umakini mkubwa, Sumaye alisema pamoja na yote aliyotendewa aliamua kuchukua fomu, kujaza na kuilipia \$1 milioni, lakini baada ya kufanya uchunguzi ameona si busara kuendelea na safari hiyo.

'Sumu haionjwi kwa ulimi'

"Inabidi leo nitangaze kuwa hiyo safari ya kugombea uenyekiti ngazi ya taifa naisitisha rasmi kwa usalama wangu, usalama wa wanachama na wa chama chenye," alisema.

"Kwa bahati nzuri alipokuwa Arusha kwenye mkutano wa kanda (Jumamosi iliyopita Novemba 29), Mbowe alishatutahadharisha kuwa sumu haionjwi kwa ulimi."

Sumaye alisema uchaguzi wa kanda na wa taifa utakofanyika Desemba 18 umeacha majeraha mengi ambayo si ya kushindwa kwenye uchaguzi bali ya mgawanyiko ndani ya chama kwa sababu walikuwa wanachaguana kwa kutegemea kundi la nani.

"Kwa wale waliokuwa Team Mbowe, kulikuwa na nguvu kubwa kutoka nje ya kanda zilizotumika na ambao siyo Team Mbowe waliumizwa sana. Hiyo hali haijengi umoja na mshikamano katika chama," alisema.

Shutuma kwa Mbowe

Sumaye alisema hakuwa na nia ya kugombea uenyekiti wa kanda, lakini akisema kuna kundi la wanachama waliokwenda kumshawishi agombee tena na ndio waliomchu kulia fomu, akaijaza na kuirejesha, jambo ambalo alisema lilimfurahisha kila mmoja.



Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye (kulia) akizungumza katika mkutano na maandishi wa habari alipokuwa akitangaza kujivua uwanachama wa Chadema, jijini Dar es Salaam jana. Picha na Ericky Boniphace

FAHAMU >

Sumaye ni nani?

Fredrick Tluway Sumaye alianza kujishughulisha na siasa mwaka 1983 na akagombea ubunge na kushinda mwaka 1985. Aliteuliwa na Rais Ally Hassan Mwinyi kuwa Naibu Waziri wa Kilimo na Maendeleo ya Ushirika wadhifa alioushika hadi mwaka 1994 alipoteuliwa kuwa waziri kamili wa wizara hiyo.

Baada ya uchaguzi mkuu wa 1995, Sumaye alishinda ubunge na kuteuliwa na Rais Benjamin Mkapa kuwa Waziri Mkuu nafasi aliyoitumikia kwa miaka yote ya 10.

Mbio za urais

Alianza harakati za kusaka urais alipoteuliwa tena kuwa Waziri Mkuu mwaka 2000 na ilipotimu mwaka 2005 wakati Mkapa anaondoka, alijitosa kuwania urais lakini akashindwa ndani ya CCM na Jakaya Kikwete.

Mwaka 2015 pia alijitokeza kugombea urais, lakini jina lake likakatwa na CCM mapema. Sumaye alihusisha kuenguliwa kwake na rushwa.

Kuhamia Chadema

Agosti 22, 2015, Sumaye alitangaza kuhamia upinzani bila ya kutaja chama na Desemba 13 mwaka huo akakabidhiwa rasmi kadi ya Chadema. Alijiunga na upinzani siku chache baada ya waziri mkuu mwingine wa zamani, Edward Lowassa kuhamia Chadema baada ya kuenguliwa kwenye urais.

Sumaye alifanya kampeni 2015 chini ya mwamvuli wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) ambao pia uliundwa na vyama vya Chadema, NCCR-Mageuzi, CUF na NLD.

Baadaye Sumaye alipewa heshima ya kuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema. Akiwa Chadema amepata misukosuko kama ya kunyang'anya mashamba yake, lakini akaendelea kusonga mbele.

Hata hivyo, safari yake iliingia dosari mwezi uliopita baada ya kujitosa kugombea nafasi mbili; kutetea uenyekiti wake wa Kanda ya Pwani na kugombea uenyekiti wa Chadema.

Katika uchaguzi huo wa Novemba 28, 2019 mjini Kibaha, Sumaye aliyekuwa peke yake alipigiwa kura 28 za ndio na 48 za hapana. Matokeo hayo yameiacha kanda hiyo ikijipanga kutafuta mwenyekiti mwingine.

"Nongwa ilikuja baada ya mimi kuamua kuchukua fomu ya kugombea kiti cha taifa. Pamoja ni haki yangu kwa katiba ya chama chetu, lakini nilikuwa na lengo la kuondoa hisia ambayo imejengeka sana katika jamii ndani ya Chadema hakuna demokrasia ya kweli," alisema Sumaye aliyekuwa Waziri Mkuu kuanzia mwaka 1995 hadi 2005.

"Lakini la pili, nafasi ya mwenyekiti taifa ni ya Mbowe tu na

haisogelevi na mtu yeyote. Mimi binafsi sikuamini hisia hizi kuwa ni za kweli ndiyo maana niliona haya yasipofutika yanatuchafulia jina la chama chetu, kumbe mimi ndiyo nilikuwa nimekosea sana kufikiri hivyo.

"Pamoja na nia hiyo njema, bada la ya busara kutumika hata kama tungetaka kumlinda Mbowe wetu, njia za ovyo ndizo zilitumika".

Pia alikuwa na ushauri kwa Mbowe.

"Ndugu yangu Mbowe najua utakuwa mwenyekiti wa chama, tafadhali uunganishe hayo makundi maana kwa jinsi ninavyowajua baadhi yao watawasumbua sana wale wengine.

"Bado natamani kuona 'chama cha upinzani kinachopishana uongozi na CCM kama ilivyokuwa kwenye nchi za wenzetu walioendelea. Lakini kwa hali hii, safari bado ndefu lakini tujitathimini kihalisia na kufanya marekebisho ya kasoro hizi na nyingine, safari inaweza kuwa fupi."

Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, ambaye ni mmoja wa watu wanaosema walimpia Sumaye fedha za kuchukulia fomu, alisema, "kuondoka kwa Sumaye kumenishitua lakini hakutaturudisha nyuma. "(Kuondoka kwa Sumaye) Kut-aongeza usiri katika vikao vyetu na ile Chadema iliyokuwa inaulizwa kuwa imerudi nyuma, sasa utaiona inasonga mbele," alisema.

"Sumaye alipaswa kusema ukweli kwa nini ameondoka si kweli kwamba ni kwa sababu kugombea nafasi ya mwenyekiti. Chama kilikuwa na mapenzi sana na yeye na ndiyo maana kilimpitisha peke yake kuwa mgombea wa nafasi ya mwenyekiti Kanda ya Pwani."

Katika mkutano wa jana, mofisa wa polisi na askari wa kawaida wenye sare walikuwepo kwenye jengo la LAPF Kijitonyama kuhakikisha ulinzi kwa mtendaji huyo mkuu wa zamani wa Serikali, tofauti na mikutano yake mingine.

Katika mkutano huo pia alikuwepo katibu wa Kanda ya Pwani, Mabina ambaye baadaye alitangaza kujiuzulu nafasi hiyo.

"(Haya) Ymetokea ndani ya eneo langu la kazi na kwa maana hiyo leo Jumatano nimewasilisha barua ya kujiuzulu nafasi yangu. Nitabaki kuwa mwanachama mwaminifu wa chama chetu," alisema.

SportPesa

www.sportpesa.co.tz

PIGA *150*87#

JINSI YA KUCHEZA

1

WEKA PESA.

- Piga *150*87#, chagua 4 - Weka Pesa.
- Fungua menyu ya Airtelmoney/Halopesa/Eazypesa
- Chagua lipa/lipia bili
- Weka namba ya kampuni 150888, Kumbukumbu 888.
- Kisha weka 500 au zaidi.

SEND

2

WEKA BET.

- Piga *150*87#

SEND

MKEKA WA EDDO



Kucheza
Piga *150*87# au tembelea
www.sportpesa.co.tz

ARSENAL V BRIGHTON

1 1.67

X 4.07

2 4.68

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:

0764115588, 0677115588
0692115588, 0685115588

18+ @TZSportPesa f @SportPesaTZ @tzsportpesa

SHINDA JACKPOT

TSH. 329,


Beki yampasua kichwa Ljungberg

London, England. Kocha wa muda wa Arsenal, Freddie Ljungberg ameitetea safu yake ya ulinzi inayovuja kama chandarua ambayo imekuwa ikisolewa na mashabiki akisema anatafuta namna ya kupunguza matukio ya kukimbizana na washambuliaji wenye kasi.

The Gunners, ambayo haijashinda mechi wa ligi tangu mwanzoni mwa Oktoba, imeruhusu mabao 21 katika mechi 14 za EPL tangu mwanzo wa msimu, idadi ambayo ni mbovu zaidi miongoni mwa timu zilizo katika nusu ya juu ya msimamo.

Kusajiliwa kwa David Luiz hakujazaa matunda yaliyotarajiwa, huku Mbrasil huyo akijumlika na Shkodran Mustafi

na Sokratis Papastathopoulos katika safu inayotajwa kuwa haina ubora wa kutosha kushindana katika soka la kiwango cha juu.



Hata hivyo, Ljungberg anaona hakuna tatizo kwa mabeki wake kuhusiana na uwezo na ufundi badala yake anasisitiza kinachotakiwa ni kuhakikisha kuwa hawaruhusu kukimbizana na wapinzani wenye kasi.

"Tunapaswa kutafuta suluhisho katika ulinzi. Kiujumla tunatakiwa kuweka mfumo ambao kila mmoja atakuwa anajua nini cha kufanya," alisema Ljungberg.

Arsenal leo itaivaa Brighton kwenye Uwanja wa Emirates.

UTATA

Dada'ke Ronaldo amchana Van Dijk

Lisbon, Ureno. Dada wa Cristiano Ronaldo, Katia Aveiro amemshukia Virgil van Dijk kwenye ukurasa wa Instagram baada ya beki huyo kutania kwamba mshambuliaji huyo wa Juventus "wala hakuwa mshindani" katika tuzo ya mwaka huu ya Ballon d'Or.

Nyota wa Barcelona, Lionel Messi aliweka rekodi ya kuwa mtu wa kwanza kutwaa tuzo hiyo kwa mara ya sita huko Paris. Ufaransa Jumatatu iliyopita, huku beki huyo wa Liverpool akimaliza wa pili katika kura zilizoamua mshindi.

Ronaldo ambaye ni mshindi mara tano wa tuzo hiyo hauhudhuria hafla hiyo, badala yake alikuwapo katika sherehe nyingine usiku huohuo ya Gran Gala del Calcio jijini Milan ambako alipokea tuzo yake ya 'Mchezaji Bora wa Serie A'.

Van Dijk alijibu swali aliloulizwa kuhusu kutohudhuria kwa straiika huyo mwenye umri wa miaka 34 katika mahojiano na televisheni ya RTL7 ya Uholanzi alipokuwa katika zulia jekundu wakati akiwasili kwenye hafla hiyo, akitania kwamba 'Ronaldo wala hakuwamo' katika

mbio za kutwaa Ballon d'Or mwaka huu.

Alipoulizwa kutohudhuria kwa Ronaldo kulimaanisha kwamba mshindani mmoja keshapungua katika jaribio lake la kutwaa tuzo hilo, Van Dijk alijibu: "Kwani alikuwa mshindani, hata hivyo?"

Kauli hiyo imemtibua nyongo dada yake Ronaldo, Aveiro, ambaye anaona Van Dijk a m e o n y e s h a dharau dhidi ya straiika huyo na akatumia ukurasa wake wa Instagram kumtaka beki huyo wa Liverpool atambue kwamba wala hayuko ngazi moja na CR7. "Sasa, dear Virgil, unakoenda, Cristiano Ronaldo ameenda na kurudi mara elfu."

"Ronaldo ni bingwa mara tatu katika nchi ambayo umesota miaka tele na hujaligusa kombe. Alikuwa mchezaji bora na mfungaji bora katika ligi unayocheza. Tena alikuwa na umri mdogo kuliko wewe. Na kuhusu hizo Ballon 'Or a n a z o tano."



02

Nafasi ambayo Virgil van Dijk alishika katika Tuzo za Ballon d'Or mwaka huu.

Biashara bado inajipanga

Dar es Salaam. Kocha wa Biashara United, Francis Baraza amesema anahitaji muda zaidi wa kuwajua wachezaji wake ili kutengeneza mpango mkakati utakaoifanya timu hiyo kuwa tishio katika mechi zilizobaki kwenye Ligi Kuu Bara.

Baraza alijiunga na Biashara United mwishoni mwa mwezi uliopita akitokea kluba ya Chemelli Sugar ya Kenya na katika mechi tatu ambazo ameiongoza timu hiyo, ameshinda mbili dhidi ya Ndanda na Lipuli na kutoa sare moja dhidi ya Mtibwa Sugar.

Kocha huyo amewapa mapumziko ya wiki moja wachezaji wake kabla ya kuendelea na mazoezi kujiandaa kwa mechi zijazo za ligi hiyo.

"Ndio kwanza hivi karibuni nimefika katika timu hii hivyo bado sijawajua vizuri wachezaji wangu kiuchezaji ili kuona tunajipanga vizuri kimbinu kuhakikisha mechi zijazo tunafanya vizuri na kupanda kwenye msimamo."

"Kadri tunavyoenda, timu itabadilika na naamini tutafanya vizuri na Mungu atatusaidia hatutashuka daraja," alisema Baraza.

Shime anataka kombe Cecafa

Dar es Salaam. Kocha wa timu ya taifa ya wasichana chini ya miaka 17, Bakari Shime amejawa na matumaini ya kufanya vizuri katika mashindano ya Chalenji ya Cecafa yanayotarajiwa kufanyika nchini Uganda kuanzia Desemba 9 hadi 19 mwaka huu.

Shime alisema wanaendelea na maandalizi ambayo yamejikita katika kuwajengea uwezo wachezaji wake wa kucheza kitimu zaidi katika mashindano hayo.

"Matumaini yapo kutkana na wachezaji nilionao, kuna vitu vidogo ambavyo tunavifanyia kazi, napenda tukacheze kitimu zaidi, itatusaidia kufika mbali na kufanya vizuri," alisema kocha huyo.

Timu hiyo ya taifa ya Tanzania ipo kundi moja Burundi na Djibouti.

Kundi lina timu za, Uganda na Ethiopia, Eritrea na Sudan Kusini. (Ellya Solomon)



Laini yako itafungwa kama hutosajili upya laini yako kwa njia ya alama ya kidole kabla ya tarehe 31 Desemba.

Tembelea wakala yeyote wa mtandao wako wa simu ukiwa na namba yako ya NIDA kusajili upya laini yako. Ni rahisi na haraka.



KUPOTELEWA NA CHETI



FANUEL CHRISTIAN MAMUYA
MTAJWA HAPO JUU AMEPOTELEWA NA CHETI CHA FORM FOUR (CSEE) MAENEO YA DODOMA SHULE: DARAJANI SECONDARY SCHOOL INDEX NO: S 1075 - 0151 MWAKA: 2015 PAMOJA NA CHETI CHA KUZALIWA TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI CHA DODOMA NA KUPEWA RB NO: DOD/DOD/RB/ 444383 / 2019

KUPOTEA KWA HATI YA URAIA.



NYAMUZIGA E. PAULO.

Mtajwa hapo juu amepotelewa na hati ya uraia wa Tanzania yenye serial namba 6380 na DN.207686 iliyotolewa mwaka 1980 na Idara ya Uhamiaji Tanzania.

Taarifa za upotevu zimetolewa kituo cha polisi na kupewa kumbukumbu namba BU/RB/526/019.

Kwa yeyote atakayeona hati hiyo atoe taarifa kituo chochote cha polisi kwa kumbukumbu namba rejea hapo juu.

KUPOTEA KWA PASSPORT



Mimi KAREEN NEMELAKI LIMBE

ninatangaza kupotelewa Na Passport No. TAE042256 iliyotolewa 07th AUG 2018 Dar es Salaam.

Yeyote atakayeona atoe taarifa kituo chochote cha police kilicho karibu kupitia Kumbukumbu namba, DAR/CEN/RB/530228/2019.

KUPOTEA KWA CHETI



BADRIYA M. KHAMIS
MTAJWA HAPO JUU AMEPOTELEWA NA CHETI CHA FORM SIX (ACSEE) MAENEO YA ILALA BOMA - DAR ES SALAAM SHULE: TUSIIME SECONDARY SCHOOL INDEX NO: S 2499 - 0666 MWAKA: 2016 TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI CHA MSIMBAZI NA KUPEWA RB NO: DAR /MSI/RB/ 52737 / 2019

KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



CYRIANUS BALYAREMWA TARAMA
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASSPORT NAMBA ABO646205 MAENEO YA MKUYUNI, BUTIMBA MWANZA TAREHE 3 DESEMBER 2019.

YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KWA RB NAMBA MWA/IGO/RB/527863/2019 AU APIGE SIMU NAMBA 0756588987 AU 0787685879.

KUPOTEA KWA KADI YA PIKI PIKI

SALIMA IDDI SHEMSANGA
MTAJWA HAPO JUU AMEPOTELEWA NA KADI YA PIKI PIKI

KADI HIYO IMEPOTELEA MAENEO YA ILALA BOMA - DAR ES SALAAM PIKIPIKI NO: MC 771 CJL AINA YA PIKI PIKI: BOXER RANGI YA PIKI PIKI: NYEUSI TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI CHA MSIMBAZI NA KUPEWA RB NO: DAR /MSI/RB/ 492007 / 2019

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

HASSAN MSHORO LUZINGA
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA GARI AINA YA NISSAN DATSUN YENYE NAMBA ZA USAJILI T. 458 AKZ NA CHASIS NAMBA CG7209223144 YENYE RANGI YA BLUE YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLIS KWA RB NAMBA MA/KIR/RB/52264/2019.

KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

BAKARI NGOMA MAKOKO.
anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj namba MC 751 BQE aina ya TVS KING iliyotolewa na TRA.

Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa kumb Na. DAR/URA/RB/52611/2019.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II (S.M.M 1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika Mahakama ya Mwanzo KIMARA Usimamizi wa Mirathi 313 / 2019 Ombi la ELIZABETH ANDREA HANGE Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu DIANAELI GADIEL MASAKI Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 11/12/2019. Kabla muombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 02/12/2019

Sahihi ya Hakimu

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU WILAYA YA GEITA

SHAU RI LA MADAI 54 2019 MDAI.....JANETH JONATHAN MOBE DHIDI YA

MDAIWAJOHN WAMBURA WANGWE WA IGUNGA TABORA AMRI

UNAAMRIWA NA MAHAKAMA UHUDHURIE HAPA MAHAKAMANI MNAMO TAREHE 19/12/2019 SAA 2:30 ASUBUHI BILA KUKOSA.

USIPOHUDHURIA SHAU RI HILI LAWEZA KUSIKILIZWA UPANDE MMOJA BILA YAWEWE KUWEPONA NA KUTOLEWA UAMUZI.

HAKIMU GEITA

KUPOTEA KWA CHETI /CERTIFICATE OF INCENTIVES MAR-KIM UNIPLAST COMPANY LTD

ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI (CERTIFICATE OF INCENTIVES) YENYE NAMBA RI 00215480 KWA USAJILI NO. 041657 KILICHOTOLEWA NA TANZANIA INVESTMENT CENTRE (TIC) TAREHE 9th AUG 2017 KWENYE KAMPUNI YA MAR-KIM UNIPLAST COMPANY LTD TAARIFA YA UPOTEVU IMETOLEWA KITUO CHA POLISI NA KUPEWA KUMB. NA. DAR/OST/RB/492489/2019. KWA YEYOTE ATAKAYEKIONA CHETI HICHO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KWA KUMBUKUMBU NAMBA REJEA HAPO JUU.

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

GODLISTEN WIL-FRED MMARI.

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari namba T623 CHZ aina ya TOYOTA NOAH iliyotolewa na TRA. Taarifa imetolewa kituo cha polisi cha kawe kwa kumb Na. KW/K/RIW.

KUPOTEA KWA KADI YA GARI VICTOR STANLAUS MASHAMBA,

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari namba T576 CBZ aina ya SUZUKI SWIFT iliyotolewa na TRA. Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa kumb Na. DAR/MSI/RB/526771/2019.

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

JAMES RANDOLIPH DARGAN,

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari namba T467 DFD aina ya SUZUKI JIMMY iliyotolewa na TRA.

Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa kumb Na. UD/RB/2310/2019.

KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI MOHAMED SAID MAGANDI.

anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki namba MC 410 BRG aina ya BAJAJ BOXER iliyotolewa na TRA. Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa kumb Na. CHA/B/20/VOL-CIXX/215.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II (S.M.M 1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika Mahakama ya Mwanzo KIMARA Usimamizi wa Mirathi 315 / 2020 Ombi la SULEIMAN SAID LUKINGA Kuteuliwa

Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu SALMA SALEHE MKWAYU Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 03/02/2020 Kabla muombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 03/12/2019

Sahihi ya Hakimu

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA YA WILAYA YA KILOSA

RUFAA YA JINAI NA. 52/2019 BAKARI MNADAMRU-FANIWA

DHIDI YA ELISHA JEREMIA BARAKA ROBERT PASCHAL ELISHA. SITE ADAMMRU-FANIWA Stephano Chilewa, Elisha Jeremia, Baraka Robert, Paschal Elisha, Site Adam, Mnaamriwa kuhudhuria Mahakamani nyinyi wenyewe binafsi au Wakili wenu mnamo tarehe 6/12/2019 kwenye shauri la Rufaa Jinai Na 52/2019. Hivyo mnatakiwa kufika bila ya kukosa tarehe hiyo. Tambueni kuwa kukosa kufika katika shauri hilo, shauri litasikilizwa bila nyinyi kuwepo.

Hati hii imetolewa leo tarehe 29/11/2019 mbele ya Mahakama ya Wilaya Kilosa.

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA WILAYA KILOSA

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA MAHALI: KIGOMA MAOMBI NA 170 YA MWAKA 2019

NTAHENGAMA ANTEPEL SHE-DRACKMWOMBAJI DHIDI YA

GEORGE JOSEPH KISANJA NA WENZAKE WAWILI.....MJBUM MAOMBI WITO/KUITWA SHAURINI KWA: GEORGE JOSEPH KISANJA NESTORY CHARLES EMMANUEL KASEKE Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 25

Mwezi wa 2 Mwaka 2020 saa 8:30 Asubuhi mbele ya Mhe. M.NYARUKA Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo

Tarehe 03 Mwezi wa 10 Mwaka 2019 Mwenyekiti

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II (S.M.M 1994 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika Mahakama ya mwanzo TEMEKE Wilaya ya TEMEKE. Usimamizi wa MIRATHI. 476/2019. Ombi la ADERA THEODORI THOMAS kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu CLECENCI HUBETI LIBEA Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 17/12/2019 kabla huyo Mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu upo mahakamani waweza kukaguliwa.

TAREHE 3/12/2019. SAHIHI YA HAKIMU.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II (S.M.M 1994 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)

Katika Mahakama ya Mwanzo BOMANG'OMBE Usimamizi wa Mirathi Namba 18 Mwaka 2019 Ombi la SAID MASOUD SAID Kuteuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi ya Marehemu SOUD SAID MASOUD Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA /VISIWANI Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu Huyo wanaalikwa kuhudhuria kesi Tarehe 17/12/2019, Kabla huyo Mwombaji hajateuliwa kuwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Imetolewa leo tarehe 03.12.2019

SAINI YA HAKIMU HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO BOMANG'OMBE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA FORM II (S.M.M 1984 NYONGEZA)

YA 5 KANUNI YA 2 Katika Mahakama ya Mwanzo BUGURUNI Usimamizi wa Mirathi 296 / 2019

Ombi la HAIKA JASPER MDINGI Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu JASPER SENZIGHE MDINGI Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 23/12/2019 Kabla muombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 02/12/2019 Sahihi ya Hakimu

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA FORM II (S.M.M 1984 NYONGEZA)

YA 5 KANUNI YA 2 Katika Mahakama ya Mwanzo BUGURUNI Usimamizi wa Mirathi 296 / 2019

Ombi la HAIKA JASPER MDINGI Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu JASPER SENZIGHE MDINGI Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 23/12/2019 Kabla muombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 02/12/2019 Sahihi ya Hakimu

EXD ✓ ↵


The approved project has fulfilled the investment requirements, which are: -

- (a) Minimum finance investment threshold has been exceeded, the project expects to invest ... US\$ 2.236m ...
- (b) Legal entity has been incorporated under certificate

No. 69352 of 10/01/2009

Based on the above, the letter of approval is hereby submitted for signature in order for the project to comply with the requirements of Section 17 of Tanzania Investment Act, 1997.

Submitted for signature.



N. A. Senzia
DIF

20th March 2009

EXD

In response to the TIC letter of registration dated 17th March 2009

the project has submitted the required documents namely: -

- (a) Company Board Resolution.
- (b) Reference letter/Financing from Source of finance LTP
- (c) lease agreement to evidence of land

With the above submission EXD is requested to sign Certificate of Incentives No. 041657 herein attached.

3/4/09

Needs

Pse process required as appropriate



DAF

Please refer to per folio 8 above

and request

19/01/2012




DIF

30

Hg DIF

Application to amend Shareholders has met requirements including BRELA evidence. I recommend draft COI be approved for signature.


 1 FY (P) 09/08/2017

4

EXB

A certificate of incentive has been awarded by adding new name of shareholder as per BRELA records. I submit for your review and signature.

~~Signature~~
10 August, 2017

APPROVED BY EXI
Sign: 
Date: 12/08/2017

5

C-DIF

Please assist the Investor as per the request in file
Customer
As. DCA-2/11/2017

1 FY (P) - FY

Share and advise

C-DIF - 27/11/17


6

MINUTE SHEET

Dokezo
No.

7 BRELA (F.S)

Kindly please authenticate the change of shareholder before we amend the certificate.

 (f.m.) 27/11/2019

MINUTE SHEET

Dokezo
No.



0223224

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

Certificate of Incentives

THIS CERTIFICATE REPLACES ^(Section 17 of the Tanzania Investment Act, 1997) THE PREVIOUS ONE NO. 041657
 ISSUED ON 2/4/09

AMENDMENT ON SECTION 1 HAS BEEN EFFECTED

No: 041657

Iskhanly

Iskhanly

This is to certify that

MAR - KIM UNPLAST COMPANY LTD

of address P.O. BOX 75498

DAR ES SALAAM

has been granted a Certificate of Incentives to invest in a new, ~~rehabilitation & expansion~~ ~~or equity of the~~ enterprise known as

MAR - KIM UNPLAST COMPANY LTD

Which is located at PLOT NO. 311, BLOCK D, MBEZI - KINONDONI

DAR ES SALAAM

Further particulars required by Section-17 of the Tanzania Investment Act are set out overleaf.

Iskhanly

Executive Director

Tanzania Investment Centre
P.O.Box 938, Dar es Salaam

Dated 9TH AUGUST 2017



This Certificate is issued in accordance with the provisions of Section 17 of the Tanzania Investment Act, 1997 and subject to the conditions prescribed under item 14 and 15 hereafter:-

1. Shareholders

	Nationality	Shareholding (%)
Akif Kara	Turkish	46
Ismail Mohamed Salim	Tanzanian	49
Mahmut A. Tekitants	Turkish	5
2. Proposed Activities: **To Establish Manufacturing Facilities For Aluminium Sheets, Bars and Glasses**
3. Sector: **Manufacturing** Subsector: **Aluminium Products**
4. Investment cost:

	Foreign USD 6.047m.	Local USD 1.189m.	Total USD 7.236m.
--	----------------------------	--------------------------	--------------------------
5. Project Financing:

	Equity USD 6.04m.	Loans USD 1.189m.	Total USD 7.236m.
--	--------------------------	--------------------------	--------------------------
6. Source, terms and conditions of loan.....
7. Assets to be invested:

	Foreign USD 6.047m.	Local USD 1.189m.	Total USD 7.236m.
--	----------------------------	--------------------------	--------------------------
8. Technology Agreement **None**
9. Date of TIC Registration: **19th March 2009**
10. Implementation period **March 2009 February 2012**
11. Operative date..... **March 2012**
12. Investment Incentive Grade: As defined in part III Section 19(1), (2) and Section 20 of the Tanzania Investment Act, 1997
 - (i) Applicable Import Duty **EAC Customs Management Act, 2004 and VAT Act, 2014**
 - (ii) Applicable with-holding Tax **As per Income Tax Act, 2004 (as amended)**
 - (iii) Eligibility of Capital Allowances **As per Income Tax Act, 2004 (as amended)**
13. Protection of Investment, Arbitration and Transfer of Foreign Currency as defined in part III Section 21, 22 and 23 of the Act.
14. Conditions attached to this Certificate of Incentives
 - (i) Date of Commencement of investment has to be notified to the Centre.
 - (ii) Certificate not to be transferred, assigned or ammended
 - (iii) Failure to commence implementation within two years invalidates Certificate
 - (iv). Failure to operate investment must be notified to the Centre
 - (v) Changes in shareholding, project activities and level of invested capital must be notified to the Centre
15. Additional conditions attached to Certificate
Finished Goods are Not Allowed Under This Certificate

Signed 
Executive Director



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

United Republic of Tanzania

Tanzania Investment Centre

Exchequer Receipt

Stakabadhi ya Malipo ya Serikali

Receipt No : **99030306137**

Received from : MAR-KIM UNIPLAST COMPANY
LTD

Amount : 1,000.00 USD

Amount in Words : One Thousand United States of
America Dollar Only

In respect of : **1403091 - Certificate of
Incentives Fees**

Bill Reference : Certificate of Incentives

Payment Control Number : **995360004024**

Payment Date : **2019-11-13 00:00:00.0**

Issued by : VENANCE MICHAEL KINGI

Date Issued : 25-11-2019 10:18:10

Signature  **For Executive Director
Tanzania Investment Centre**

Government Payment Gateway © 2017 All Rights Reserved (GePG)

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS
TANZANIA POLICE FORCE



LOSS REPORT

DAR/OST/RB/492489/2019

This is to certify that

INGIA C MDING'I

Reported to the police on 21/11/2019 that the under-mentioned property/properties has been lost:-

Property Type	Property Name	Property Number
Documents(eg.School,Car Card)	certificate of incentives	041657

More Details

kimepotea

Control Number :: 9910810771225

INSPECTOR GENERAL OF POLICE (IGP)
11/21/2019 12:40:05 PM

